

**CHUKA**



**UNIVERSITY**

---

**UNIVERSITY EXAMINATIONS**

**EXAMINATION FOR THE AWARD OF DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION**

**KISW 323: MBINU ZA UHARIRI KATIKA KISWAHILI (EDITORIAL METHODS IN KISWAHILI)**

**STREAMS: B.ED (SB)**

**TIME: 2 HOURS**

**DAY/DATE: TUESDAY 06/08/2019**

**11.30 A.M. – 1.30 P.M.**

---

**MAAGIZO:**

- **Jibu swali la kwanza na mengine mawili**

1. (a) Umeajiriwa kama mhariri katika shirika la Daily Nation. Kwa kutumia alama faafu za uhariri, ifanyie uhariri Makala ifuatayo. (alama 20)

**NYIMBO ZA WATOTO NA MAENDELEO YA SAYANSI NA TEKEKNOLOJIA**

Kati ya vipindi Ambavyo havitasahaulika katika historia ya fasihi ni KARNE ya ishirini na moja, ambapo imeshuhudia kuingia kwa mambo mengimapya yenye kujikita katika urahisishaji wa kiutendaji wa fasihi. Mambo haya mapya yali yoleta mabadiliko mapya yanayoendeshwa na binadamu, yanaendelea kuenea na kuimarika kwa kiwango cha juu katika jamii kila siku, na yamepata mashiko na mwelekeo unaojulikana na wengi kuwa ni utandawazi. Utandawazi huu upejitanza hata kaatika taaluma, ambapo binadamu amejitahidi katika kuvumba mambo mbalimbali mapya, yenye kuivutia jamii, yakushangaza na yenye kuonekana ya kiubunifu wa hali ya juu sana

Malengo ya Makala hii ni kuzitathmini nyimbo za watotokatika kipindi hiki cha maendeleo ya sayansi na teknolojia mpya, fasihi ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo mwanzilishi wa fasihi andishi ya watoto, kutokana na UKWELI KWAMBA, utanzu huu unakuwa mpya kila mabadiliko yanapotokea.

Fasihi ni matokeo ya shughuli za jamii, huibuka, hukua na kusambaa kutokana na mazingira yaliyoko katika jamii na kuizunguka jamii hiyo. Hapa tunamaanisha kuwa, mwanadamu katika muktadha wa kuyakabili mazingira yanayomzunguka, amejikuta akiangukia katika ulimwengu wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia bila ye ye mwenyewe kujitambua. Vilevile amejikuta akiingia katika maendeleo ya sayansi na teknolojia bila ya ye ye kufahamu kuwa yametokana na ubunifu wake mwenyewe yenyе kuyumbuka. Kutoka na hayo, matu mizi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia katika uzalishaji wa kazi za fasihi yanaweza kutazamwa kwa jicho cha pekee katika Makala haya na kuona kama maendeleo haya yanaweza kutazamwa kwa jicho cha pekee katika Makala haya na kuona kama maendeleo haya yanaweza aidha kuboresha ama kudumaza majukumu ya utanzu huu wa fasihi simulizi

Nyimbo za watoto kama mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi zinayo majukumu yenyе mwelekeo majukumu ya utanzu huu wa fasihi simulizi

Nyimbo za watoto kama mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi zinayo majukumu yenyе mwelekeo muhimu wa kujenga mahusiano mio ngoni mwa watoto na kwa jamii nzima.

Mashirika mbalimbali ya Kidini, Asasi mbalimbali za kijamii, (fasihi ikitajwa) yameonesha wasiwasi wao juu ya kuathiriwa kwa nyimbo za watoto kutokana na mabadiliko hayo ya sayansi na teknolojia.

- (b) Bainisha umuhimu wa kozi ya mbinu za uhariri kwa mtaalamu wa uhariri. (alama 10)
  
  - 2. Eleza changamoto zinazowakumba waandishi wa vitabu vya Kiswahili nchini Kenya. (alama 20)
  
  - 3. (a) Eleza dhana ya ‘Habari’. (alama 2)
  
  - (b) Onyesha sifa mahususi zinazobainisha taarifa kuwa na thamani ya habari. (alama 18)
  
  - 4. Tathmini hatua muhimu ambazo mswada hupitia hadi kuwa kitabu. (alama 20)
  
  - 5. Kwa kutoa mifano, onyesha jinsi mhariri wa magazeti anavyotumia alama mbalimbali za uhariri kutekeleza wajibu wake. (alama 20)
-